**Learning by Ear 2010**

**Theme: Illiteracy and education**

**“A GIRL FINISHING SCHOOL”**

**Episode 09:** “*Papa Wali gizani’’*

**Author:** Frédéric Gakpara

**Editor:** Yann Durand

**Translator:** Anne Thomas

**Characters:**

**Elinam:** *(ana umri wa miaka 22 , mtoto wao Papa Wali na Mamoua, na ni kaka yake Latifa. Amehitimu hivi karibuni kwa shahada ya uzamili kwenye somo la uhandisi. Bado hajaajiriwa na angali anaishi jijini alikosomea chuo kikuu ambako ni kilomita kiasi 120 kutoka katika mji mdogo wanakoishi wazazi wake. )*

**Papa Wali** *(Ana umri wa miaka 55 na ni baba wa watoto wanne- Elinam, Latifa, Jaurés na Inés. Anashughulika na karakana ya vyuma lakini hajui kusoma na kuandika. Biashara yake imekuwa ikimwendea vibaya hivi karibuni kwa kukosa vifaa vya kisasa na usimamizi mbaya wa masuala ya kifedha na utangazaji wa kibiashara. Sasa hivi anakaa nyumbani kwa sababu ana matatizo ya macho.)*

**Mamoua** *(Mwenye umri wa 39 , mke wa Papa Wali na mama wa watoto wanne. Hajui kusoma na kuandika na ni mke-nyumbani. Anafanya biashara ndogo ya kuuza uji wa unga wa mahindi mbele ya nyumba yao.)*

**Epiphane** *(Ana umri wa miaka 21 na ni mfanyikazi wake Papa Wali. Ni kijana mwerevu sana.Amebadilisha hali ya karakana yao na inaendelea kuimarika, hayo yote ameyatenda kutoka na madarasa yake ya jioni ya kujifunza kusoma na kuandika na pia mafunzo ya ziada aliyopata kuhusu ufuaji vyuma.)*

**Zakia** *(Mwanamke mwenye umri wa miaka 23, ni mwanamke mwenye uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki wa dhati wa Latifa na ni mkurugenzi wa utangazaji wa shirika lake la Safari za Kitalii na angali akifanya kazi katika mji mdogo ambao yeye na Latifa wanatoka. Hivi karibuni, Elinam, kaka yake Latifa, amekuwa akimwandama akimtaka wawe na uhusiano wa kimapenzi.)*

**INTRO**

**Hujambo na karibu kwenye sehemu ya tisa ya kipindi cha NoaBongo-Jenga Maisha yako, mfululizo wetu wa makala ya "Mtoto wa kike ahitimu shuleni" inayoelezea elimu na kutojua kusoma na kuandika.**

*Siku nne baada ya Elinam kumuelezea Zakia hisia zake,Elinam alisafiri kuelekea kwenye mji wao mdogo wanakokaa wazazi wake, ambako aliondoka kiasi cha miaka mitano iliyopita. Zakia amesusia kupokea simu za Elinam na kwasababu hiyo Elinam ana wasiwasi hajui mambo yatakavyokuwa. Zakia hana habari kwamba Elinam yuko safarini. Je atamfikiria vipi?*

*Elinam pia hajawaarifu jamaa zake kwamba anakwenda nyumbani; kwa hivyo wazazi wake wanashangaa pindi anapowasili. Asubuhi hiyo mamake Elinam yumo kwenye kibanda chake cha kuuza uji. Afya yake imezorota na amedhoofika hana nguvu ya kufanya biashara.Hasira zake bado hazijesha. Elinam anapowasili nyumbani kwao, anampata Papa Wali akiwa kitandani anaugua. Jiunge nasi usikilize sehemu ya tisa iitwayo : "***Papa Wali haoni vizuri***".*

**Scene 1, AT PAPA WALI'S HOUSE**

Elinam na Mamoua

1. **ATMO: COURTYARD NOISES: HENS - SHEEP - BIRDS – NOT MUCH TRAFFIC**
2. **SFX: A TAXI STOPS – SOUND OF DOORS – TRUNK BEING OPENED – LUGGAGE BEING REMOVED.**

3. **Mamoua:** (**Shouting**) Ah! Ah! Ah! Elinam! Ni wewe au ninaota? Karibu! Mwanangu!

4. **SFX:** **SOUND OF SLOW DRAGGING FOOTSTEPS (old woman) – SOUND OF NORMAL FOOTSTEPS (her son) converging**

5. **Elinam:** Mama… Subiri, nitwae mikoba.

6. **SFX:** **TRUNK BEING CLOSED – CAR STARTS UP**

7. **SFX:** **SOUND OF CHAIRS BEING MOVED**

8. **Mamoua:** Keti. Nitakuleta maji.

9. **SFX:** **SOUND OF FOOTSTEPS (MAMOUA) DRAGGING IN THE ROOM – GOING AWAY – COMING BACK**

10. **Mamoua:** Maji haya!

11. **SFX:** POURING WATER INTO GLASSES

12. **Elinam:** Asante, mama! (**Drinks for a long time**) Mama, u hali gani?

13. **Mamoua:** Ningali hai, kwa rehema zake Mungu. Na wewe huna neno?

14.**Elinam:** Sina neno, nashukuru. Lakini... naona umeshapata mvi?

15.**Mamoua:** Kazi na uchovu huzeesha, mwanangu... Lakini nambie. Umefikia wapi na masomo yako? Lini utaajiriwa? Ningependa nionje mshahara wako kabla sijaondoka duniani!

16.**Elinam:** Nimeshamaliza masomo yangu. Hivi sasa natafuta kazi.

17.**Mamoua:** Tafuta kazi ya kukukimu kiasi, inayotosha kukulisha kisha uowe.

18.**Elinam:** Mhh.. **(changing the subject)** Kwani hamtumii sebule tena? Kwa nini kila kitu hapa ni kichafu?

19.**Mamoua:** Ninajihisi mchovu sana wala siwezi kufanya kila kitu. Sina mtu wa kunisaidia kwa kuwa Latifa aliondoka.

20.**Elinam:** Na Souleyman je? Mbona hasaidii?

21.**Mamoua:** Haonekani hapa mara nyingi. Anajua tu kwenda jikoni kutafuta chakula.

22.**Elinam:** Na unamwambia nini? Nasikia hata masomo amekatiza.

23.**Mamoua:** Nimwambie nini mimi? Ni mvulana hapo alipo!

24.**Elinam:** Hivyo wasema nini mama? Nilikuwa katika chuo kikuu, na niliwafundisha wanafunzi wa shule ili nijipatie kiasi cha fedha kinachotosha kujilipia kodi, nikirudi nyumbani kwangu najipikia chakula, nidurusu kabla ya kulala. Nilikuwa nikiamka asubuhi na mapema. Nilikuwa nikisafisha chumba changu na mwishoni mwa juma nilikuwa nikitumia muda mwingi kufua nguo zangu. Kwani mimi si mvulana?

25.**Mamoua:** Kwani mdogo wako Latifa hakusaidii?

26.**Elinam:** Bila shaka, alinisaidia. Lakini na yeye pia alikuwa akisoma na akikesha kuwatizama wagonjwa. Hata hivyo, yeye alikwenda madukani na kufanya kazi zangu wakati ambapo sikuwa na nafasi ya kuzifanya.

27.**Mamoua:** Haya basi, kwa vile umeshafika, zungumza na mdogo wako.

28.**Elinam:** Wajua? Umemtendekeza sana mama kiasi kwamba hamsikilizi yeyote.

29.**Mamoua:** **(sighing in a sad way)** Hm …

30.**Elinam:** Na baba jee?

31.**Mamoua:** Amekuwa kitandani kwa wiki kadhaa. Macho yake hayamudu mwangaza mchana. Haoni vizuri.

32.**Elinam:** Na hakuna mmoja wenu aliyefikiria kunipigia mimi simu au Latifa kutujulisha hali yake?

33.**Mamoua:** Hatukutaka kuwatatiza.

34.**Elinam:** Na madaktari wanasema nini?

35.**Mamoua:** Hataki kwenda hospitalini.

36.**Elinam:** Ati nini? Yuko wapi?

37.**Mamoua:** Chumbani. Nitakwenda kumuita...

**MUSIC**

**<u>Scene 2, AT PAPA WALI'S HOME</u>**

Elinam na Papa Wali

38.**SFX:** **FOOTSTEPS (ELINAM) DRAGGING ON THE GROUND**

39.**Papa Wali:** (**in a tired voice**) Karibu, mwanangu!

40.**Elinam:** Baba, mbona hujenda hospitalini?

41.**Papa Wali:** Nimechelewa, mwanangu. Sina tena cha kupona.

42.**Elinam:** Siamini kuwa hizo ni kauli za daktari.

43.**Papa Wali:** Hili tatizo limekuwa likinivamia taratibu. Rafiki ya mdogo wako Latifa, yule anayeshughulika na watalii, kiasi miaka mitatu iliyopita alinileteа vifaa vya kujikinga na miale ya moto wa kuchomelea vyuma... nilivipuuza nikidai kwamba ujuzi wangu wa kazi unatosha... sasa matokeo ndiyo haya.

44.**Elinam:** Kwa hivyo umeamua kujiacha ufe? Ni sawa na kujiua!

45.**Papa Wali:** Hapana, sivyo hivyo. Nimekata tamaa.

46.**Elinam:** Na vipi karakana?

47.**Papa Wali:** Epiphane anasimamia mambo. Ni mfanyikazi mzuri sana. Mzuri zaidi yangu mimi! Ameiimarisha biashara nzima. Ni kijana mzuri sana na nina imani naye si haba.

48.**Elinam:** Sawa, mambo ni mazuri angaa kidogo! Ningetaka kukupeleka hospitalini kesho asubuhi.

49.**Papa Wali:** Itasaidia nini?

50.**Elinam:** Tutasema angalau tulijitahidi.

51.**Papa Wali:** Sawa basi…

52.**Elinam:** Vyema. Nitakwenda kwenye karakana sasa hivi. (**Getting up**) Nataka nijue ikiwa yote yanayosemwa kumhusu Epiphane ni ya kweli. Pia ninataka kumtembelea Zakia afisini kwake.

53.**Papa Wali:** Msalimie... Lakini usimwarifu kuhusu hali yangu. Alijitahidi kunisaidia lakini nikampuuza. Sasa hivi ninahisi vibaya kwa sababu ya ukaidi wangu.

54.**Elinam:** (**A bit drily**) Si ukaidi tu, Baba. Kwa mfano, ungeweza kujiunga na masomo kama alivyofanya Epiphane. Lakini uliamua mambo vingine. Hayo ndiyo matokeo yake !

55.**Papa Wali:** (**Silence**) …

56.**Elinam: (Apologetic.Realising that he'd been carried away by emotion**)..samahani…niwie radhi Baba**..(More calmly**) Sawa, bora niondoke. Tutaonana baadaye, Baba!

57.**Papa Wali:** (**Silence**) …

58.**SFX ATMO: SOUND OF STEPS GOING AWAY (ELINAM)**

59.**NARRATOR:** *Elinam anataka kuitimiza dhamira ya ziara yake:kunusuru kinachowezekana-familia yake,biashara ya babake,na pia penzi lake kwa Zakia. Ameshampata Epiphane kwenye karakana na hivi sasa wako kwenye mlango wa afisi ya Zakia. Lakini ni Epiphane pekee aliyejitambulisha kwenye eneo la mapokezi na Zakia anapigwa na butwaa anapomuona Elinam...*

**Scene 3, AT ZAKIA'S OFFICE**

Elinam, Epiphane na Zakia

60.**SFX ATMO: OFFICE SOUNDS (UNCLEAR VOICES – PHONES RINGING – PRINTERS)**

61.**Zakia:** **(surprised)** Vipi mambo Epiphanie!

62.**Epiphanie:** Hujambo, Zakia!

63.**Zakia:** Aka! Elinam!

64.**Elinam:** Vipi Zakia?

65.**Zakia :(stuttering, ill at ease)** Una… unafanya nini hapa?

66.**Elinam:** Mwenyewe umesusia kupokea simu zangu na nilijua lau ningesema kwamba nipo kwenye mapokezi, hungekubali kuzungumza nami... Je ninaruhusiwa kuketi?

67.**SFX: PULLING CHAIR, SITTING DOWN (RUSTLE OF CLOTHES)**

68.**Zakia:** Umewasili lini huku?

69.**Elinam:** Nimewasili hivi punde.Nimeiweka mikoba yangu nyumbani kisha nikatoka.

70.**Zakia:** Na Latifa je?

71.**Elinam:** Hajambo! Lakini sikuja naye.

72.**Zakia:** **(changing the subject)** Kuna joto asubuhi hii. (**To Epiphane**) Epiphane hujambo?

73.**Epiphane:** Sijambo, dadangu!

74.**Zakia:** Na vipi mwajiri wako?

75.**Epiphane:** Hajambo, dadangu!

76.**Elinam:** Zakia, kwani hajakwambia kwamba Baba ni mgonjwa?

77.**Zakia:** **(surprised)** La, hajaniambia. Tangu lini?

78.**Epiphane:** (**Embarrassed**) … Amekuwa mgonjwa tangu miezi miwili iliyopita...

79.**Zakia:** **(shocked)** Lakini… Epiphane, kila ninapopitia kwenye karakana wewe huniambia kwamba katoka.

80.**Epiphane:** Alinikanya kuwaambia watu kwamba ni mgonjwa.

81.**Zakia:** Kwa hivyo ukaamua kutomwambia mtu yeyote? Ana nini?

82.**Epiphane:** Haoni vizuri…

83.**Zakia:** Mungu wangu! Hata sishangai, Elinam. Babako hakuwahi kuvitumia vifaa vya kujilinda alipokuwa akifanya kazi kwenye karakana yake. Vipi yu hali mbaya?

84.**Elinam:** Nitampeleka hospitalini kesho ili tujue mbivu na mbichi.

85.**Zakia:** (**Very surprised**) Kwani bado hajaenda hospitalini?

86.**Elinam:** (**Sighing**) Tuyawache hayo ya baba, tafadhali. Nimekuja kuzungumza nawe.

87.**Zakia:** (**A silence**) Elinam, usiniambie kwamba unataka kuyazungumza hayo hapa?!

88.**Elinam:** Ndiyo, ninayachukulia kuwa ni mambo ya dharura! (**To Epiphane**) Epiphane, rudi kwenye karakana. Tutaonana kesho tukijaliwa, au siyo?

89.**Epiphane:** Sawa, kaka. Kwaheri dada!

90.**SFX:** **NOISE OF CHAIR AS SOMEONE STANDS UP**

91.**Zakia:** Kwaheri, Epiphane!

92.**SFX:** **FOOT STEPS (EPIPHANE) WALKING AWAY – AN OFFICE DOOR OPENS AND CLOSES**

93.**Zakia:** (**Sighing**) Ninakusikiliza…

94.**Elinam:** Nimesubiri juma zima nikitaraji ungenipigia simu – lakini nimeambulia patupu.

95.**Zakia:** Nimekuwa na kazi nyingi sana juma hili!

96.**Elinam:** Kazi nyingi kiasi chako kususia simu zangu?

97.**Zakia:** Elinam, siwezi kujiingiza kwenye uhusiano wa kimapenzi kwa siku moja tu. Ninahitaji muda kulifikiria suala hilo. Na usisahau kwamba wewe ni kakake rafiki yangu wa dhati. Je huoni kuwa hali itakuwa mbaya endapo mambo hayatatengemaa?

98.**Elinam:** Ndipo nikachukua muda mrefu kuamua niliyoamua. Kwani unadhani siwezi kuuzingatia kwa dhati uhusiano huu?

99.**Zakia:** Elinam, mimi pia ninahitaji muda kulitafakari suala hili. Nani kasema kuwa mimi na wewe ni lazima tuwe wapenzi?

100. **Elinam:** Nimekuja kukuthibitishia mapenzi yangu kwako. Siondoki mjini hapa bila wewe!

101. **Zakia:** Una hakika ulisemalo?

102. **Elinam:** Kwani, tayari umeshaumizwa moyo?

103. **Zakia:** Si mimi niliyeumizwa! Mamangu, ndiyo! Siko tayari kujiingiza mahali bila kwanza kuchunguza hatari iliyopo.

104. **Elinam:** (**With emphasis)**Zakia. Siwezi kukuumiza moyo.

105. **Zakia:** Elinam, tusiyaharakishe mambo. Hatujaonana kiasi miaka mitano hivi. Tunapaswa kwanza kufahamiana vyema kisha mengi yatafuata. Nadhani huo ni uamuzi wa busara.

106. **Elinam:** (**Reassured**) Sawa! Ninakuahidi sitakuvunjia heshima.Popote utakapokuwa nami nitakuwa papohapo. Kwa raha na pia huzuni,vyote vyangu !

107. **Zakia:** Asante. Naomba nikusindikize hadi kwenye eneo la mapokezi. Nina kazi kibao za kufanya kabla ya kwenda kwa chakula cha mchana!

108. **Elinam;** Usiwe na wasiwasi, sitapotea njia!

109. **SFX ATMO:** **NOISE OF CHAIRS – STEPS GOING AWAY (ELINAM)**

110. **Zakia:** Asante! Nitakupigia simu baadaye!

111. **Elinam:** (**Smiling**) Una hakika?

112. **Zakia:** (**Laughing**) Naam, kweli nina HAKIKA!

113. **Elinam:** Basi tutawasiliana baadaye!

114. **SFX ATMO:** **OFFICE DOOR OPENS AND CLOSES**

115. Zakia: (**She sighs**)

**MUSIC**

**OUTRO**

*Ziara ya Elinam inaonekana kuwa ya mafanikio. Usiku huo yeye na Zakia walizungumza kwa simu kwa muda mrefu. Zakia alimuazima pikipiki yake kwendea madukani wakati yeye (Zakia) akiwa kazini. Uhusiano wao unaonekana unaendelea vizuri. Papa Wali hawezi kuwaona hao wapenzi wawili. Matibabu yake hospitalini hayakumfaa chembe.*

*Lakini Mamoua anawaona vyema wapenzi hao. Je ataukubali uhusiano huo? Hajawahi kumpenda Zakia. Elinam atafanya nini kudhibiti hali ya mambo? Na je Latifa atakoma kujisikitikia?*

*Ili kufahamu zaidi, sikiliza sehemu ya mwisho ya **"Mtoto wa kike ahitimu shuleni",** mfululizo wa mala inayohusu elimu na kutojua kusoma na kuandika.*

**Ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au vyengine vya mfululizo wa Noa Bongo-Jenga Maisha Yako,tazama mtandao wetu wa wavuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe:Anuani ni :** lbe@dw-world.de.Tunalikunja jamvi hapo kwa leo.Hadi wakati mwengine,kwaheri!

**END OF 9TH EPISODE**